THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION

021

# KISWAHILI

*(Kwa Watahiniwa Walioko na Wasiokuwa Shuleni)*

**Muda: Saa 3** **Alhamisi Novemba 04, 2004 asubuhi**

---

*Maelekezo*

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C, D na E.

2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A, B, C na D na maswali **mawili (2)** kutoka sehemu E. **Swali la 13** ni la lazima.

3. Zingatia maagizo ya kila sehemu na ya kila swali.

4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** kwenye chumba cha mtihani.

5. Mashine za hesabu za elektroniki **haziruhusiwi** kwenye chumba cha mtihani.

6. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

*Karatasi hii ina kurasa 6 zenye maandishi.*

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU A (Alama 10)

### UFAHAMU

1. Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu maswali kwa kuandika herufi ya jibu sahihi katika karatasi ya kujibia.

Nilizaliwa na nasaba bora. Mbingu ni baba yangu na ardhi ni mama yangu. Tangu utotoni, mchana nimevaa nuru na usiku nimejifunika giza. Kinyume na viumbe wengine nala kwa miguu, badala ya kutembelea. Hii ndiyo desturi yetu sisi miti. Kinywa hutumika kwa kusema tu, kama kifanyavyo leo kwa kusimulia hadithi ya maisha yangu. Mtaona ajabu lakini ndivyo nilivyoumbwa. Nami najivuna kama wajivunavyo viumbe wengine.

Nilianza maisha yangu miaka thelathini iliyopita. Huu si umri mkubwa kwa mti. Lakini ni mkubwa wa kutosha mkisikia mambo yaliyonisibu. Nilipokuwa na umri wa miaka mitano, mvua haikupatikana. Watu walianza kudhikika na nikakaribia kufa.

Umri wangu ulipokuwa miaka kumi, palitokea dhoruba kali sana. Miti iling'oka na nyumba kadhaa zikaharibika. Mimi peke yangu ndiye niliyejizuia kwa nguvu zangu zote. Kusema kinaganaga niliokoka kufa tu si majeraha. Tawi langu moja lilivunjika, nikapata uchungu mwingi sana. Wakati lilipokuwa likianguka, lilipiga nyati aliyekuwa chini ya kivuli changu, watu wakapata nyama ya kula. Tangu siku ile, tukio hilo liliamsha hisia za ushirikina miongoni mwa watu. Mtu mmoja aliyezoea kuabudu mizimu, alianza kuniabudu maana mti aliokuwa akiabudu kabla uling'oka.

Kwa kumfuasa mtu huyu, watu wengine walianza kuniabudu vilevile. Sijui kwa nini. Mwaka uliofuata mvua nyingi ilinyesha; watu wakafurahi sana. Baadhi yao waliamini kwamba mvua ile ililetwa na ibada yangu, nikafanywa mzimu mkubwa. Katika mwaka wangu wa kumi na tano palikuja hatibu mkubwa sana mjini, kivuli changu kikachaguliwa kuwa mahala pa mazungumzo ya dini. Watu wa pande zote walikuja nikawa mahali pa kama Jerusalemu na Makka.

Tamasha kubwa za dini zilifanywa chini yangu nikawa katika utukufu kwa muda wa miaka kumi na mitano mfululizo. Mambo yaligeuka. Siku moja watoto walikuwa wakicheza bui katika mti uliokuwa karibu na mimi. Waliendelea wakacheza mchezo huo kwenye matawi yangu. Watoto kumi walisimama juu ya tawi moja. Tawi lilivunjika kwa sababu ya uzito wao, watoto wawili katika hao wakapoteza maisha. Watu walichukizwa na tukio hili lakini waliendelea kuniabudu. Palikuwa na shida ya mvua katika mwaka huo huo. Na baya kuliko yote ilikuwa ni ajali ile iliyotokea kwa watoto wale wawili. Tangu siku ile watu walinituhumu kwamba mashetani waovu walikuwa katika shina langu.

Basi watu waliacha kuniabudu. Watoto hawakuja tena kucheza karibu yangu. Watu walikasirika sana hata wakaanza kunitendea maovu. Majani yangu yalipasuliwa, maua yangu yaliyokuwa yakinuswa na kutunzwa kama hirizi, yalikanyagwa chini, matawi yangu yalikatwa, shina langu likaharibiwa sana kwa kukerezwa na kuchomwa moto.

Heri na shari zangu katika maisha ni hizi. Nimesimama hapa kungojea mauti. Nimetendewa jeuri, nimeshambuliwa, tena nimetiwa katika huzuni isiyovumilika. Kinyume kilioje? Kwanza nilipewa sadaka, sasa napata mashaka. Kwanza nilikuwa mahali pa haji, sasa pamekuwa mahali pa mashetani waovu.

### MASWALI

(i) Kichwa cha habari kinachofaa kwa kifungu hiki ni

A imani za kishirikina
B maisha ya mtu
C matatizo yanayomkabili binadamu
D tahadhari ya maisha kwa binadamu
E maumbile ya viumbe hai.

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

(ii) Hali ya upekee inayomfanya mhusika kujivunia ni

A kuzaliwa na nasaba bora
B kuwa na kinywa cha kusema tu
C kula kwa miguu badala ya kinywa
D kuabudiwa na kuteuliwa kuwa mahala pa mazungumzo
E kuwa katikati ya mbingu na ardhi.

(iii) Desturi ya miti ni

A kula kwa miguu badala ya kinywa
B kinywa hutumika kwa kusema tu
C kusimulia hadithi ya maisha ya miti
D kujivuna kama wajivunavyo viumbe wengine
E miguu kuwasaidia kujieleza.

(iv) Kusema kinaganaga niliokoka kufa tu, si majeraha. Hii ina maana

A vifo vya watoto wawili viliwakasirisha watu hata wakaanza kuutendea maovu ule mti
B mti haukupendezwa na ibada za kishirikina
C mti ulitumia nguvu zake zote kujinusuru usiangushwe na dhoruba
D tawi lake moja lilivunjika akaona uchungu mwingi sana
E wanyama walinionea huruma kwa mateso yaliyonipata.

(v) Sababu iliyowafanya watu waendelee kuabudu mti ulioleta maafa ni

A hapakuwa na mti mwingine wa kuabudu
B palikuwapo na shida ya mvua mwaka huo huo
C kutokana na mti huo kufanywa mzimu mkubwa
D kuwa mahali pa haji kama Jerusalemu na Makka
E mti huo ulikuwa na matunda yaliyosaidia kwa chakula.

(vi) Kipindi cha utukufu cha mti huo kilikuwa

A miaka thelathini iliyopita
B miaka kumi na tano mfululizo
C miaka kumi
D miaka kumi pamoja na mwaka uliofuata tukio
E mara tu baada ya kupatikana kivuli.

(vii) Msemo wa kufa kufaana umejidhihirishaje katika habari hii?

A Miti iling'oka na nyumba kadhaa kuharibika
B Watoto walipata mahali pa kucheza bui
C Mti usiokumbwa na dhoruba tawi lake liliua nyati
D Mashetani waovu walifanikiwa kuingia katika shina la mti wakati watoto wanacheza
E Mti ukafa na watu wakapata kuni.

(viii) Watu waliacha kuabudu katika mti ule kwa sababu

A walikasirika sana
B mti huo ulisababisha vifo
C waliamini kuwa ndicho chanzo cha vifo vya watoto wawili
D shida ya kutokuwa na mvua ilishakwisha
E. majani na matunda ya mti vilikuwa na sumu.

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

(ix) *Neno 'hatibu' katika aya ya nne lina maana ipi?*

A *Katibu*
B *Mheshimiwa*
C *Mtu maarufu anayetangaza*
D *Mhubiri*
E *Mfanyabiashara.*

(x) *Heri ya mti wakati wa maisha yake ni pamoja na*

A kupewa sadaka kwanza na kisha kupewa mashaka
B kufanywa mahali pa haji na kutolewa sadaka
C kuwa mahali pa haji na baadaye pa mashetani
D kusimama kungojea mauti
E kuna wanyama kwa ajili ya kitoweo.

2. Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha **andika ufupisho wa maneno 60** kuhusu habari hiyo.

"Harusi hii ilikuwa ifanyike wakati Ashura alipomaliza kidato cha nne, lakini Ashura huyu ametufanyia uhuni na vituko visivyoelezeka. Hali hii imetufanya kijiji kizima kituchukie. Tunatungiwa nyimbo na hatuna raha. Tumekuja kukuomba ili umfukuze shule na hilo litamaliza kiburi chake. Sisi tuko tayari kukulipa kiasi chochote cha fedha ukitimiza haja yetu hii." Mzee Juma akiwa ameongozana na mkewe walieleza.

Mwalimu mkuu alitafakari kisha akauliza "Ashura ana kiburi kumbe?" Mama Ashura alijibu "Usimwone hivi. Ashura hataki kufuata utamaduni wetu wa kuolewa. Anataka ati achague mchumba mwenyewe, na mahari haoni kuwa ni kitu cha msingi. Kiburi hicho kinatokana na elimu mliyompa shuleni. Anafanya apendavyo. Eti naye anatoa ushauri. Elimu gani isiyojali adabu na utii?"

Hapa mwalimu aliona kwanza awaelimishe kabla hajawatolea kauli ya mwisho. Alikwishatambua kwamba wazazi wa Ashura walikuwa wameachwa nyuma na wakati. Kila upya wa mawazo waliuita kiburi.

## SEHEMU B (Alama 20)

## UTUMIZI WA LUGHA

3. Chagua kifungu cha maneno kutoka **ORODHA B** kinachotoa maelezo sahihi ya maneno/neno katika **ORODHA A**. Andika herufi ya jibu sahihi kando ya namba ya kipengele cha swali katika kijitabu chako cha kujibia.

**ORODHA A**

(i) Atakuja
(ii) Kinyonga kina uwezo wa kubadilisha rangi
(iii) Kimkang'ata
(iv) Ukwasi
(v) Wingi wa nyumba

**ORODHA B**

A Ni sentensi shurtia
B Atakuja lina mofimu nne
C Ni sentensi yenye kosa la kisarufi
D Ni rejesta ya Tanga
E Ni utajiri
F Ni ufukara
G Ni nyumba
H Ni umasikini
I Atakuja lina mofimu tano
J Ni lahaja ya Kiswahili

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

4. Sentensi zifuatazo ni tata. Toa maana mbili ili kuthibitisha utata huo.

(a) Nimenunua paa.

(b) Usisahau kuchukua pamba.

(c) Ukija njoo na nyanya.

(d) Ninakuomba usinivunjie nyumba yangu.

(e) Daktari ataniunga mkono.

5. Taja mambo **matano (5)** ya kuzingatia wakati wa utungaji wa dayalojia.

## SEHEMU C (Alama 20)

## SARUFI

6. Onesha aina **nne (4)** za vielezi kwa kutoa maana ya kielezi na kisha kuandika sentensi ya kila aina ya kielezi na kipigie mstari.

7. Ainisha maneno **kaa** na **tupa** katika sentensi zifuatazo:

(a) Tafadhali kaa hapa unisubiri.

(b) Nolea tupa kisu chako.

(c) Watu wengi hula kaa.

(d) Kama umeshiba tupa kilichobaki.

(e) Ukila kaa chini usisimame.

8. Tunga sentensi na kupigia mstari mofimu "**ki**" yenye dhima zifuatazo:

(a) Kuonesha mtendwa jambo.

(b) Kuleta upatanisho wa kisarufi.

(c) Kuunda mzizi wa kitenzi.

(d) Kuonesha masharti.

(e) Kuonesha idadi ya umoja.

9. Eleza kwa kutumia mifano maana ya:

(a) Shina.

(b) Shamirisho.

(c) Chagizo.

(d) Njeo.

(e) Kundi nomino (KN).

## SEHEMU D (Alama 10)

## HISTORIA YA LUGHA

10. Eleza kwa ufupi, sababu **tano (5)** zilizosaidia kuenea kwa Kiswahili nchini Tanzania **kabla ya** Uhuru.

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU E (Alama 40)

## FASIHI

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii. Swali la **13** ni la lazima.

11. Fasihi simulizi ina sifa gani za pekee zinazoitofautisha na fasihi andishi?

12. Sanaa ya ushairi inapevushwa kwa kutumia:

    (i) Mtindo na muundo. (ii) Lugha na matumizi ya picha.

    Jadili vipengele hivyo kwa kutumia washairi wawili kati ya walioorodheshwa.

13. Kwa kutumia riwaya mbili zilizoorodheshwa, onesha uhalisia wa dhamira **nne (4)** kwa jamii.

14. Taja maadui **sita (6)** na fafanua jinsi waandishi wa tamthiliya mbili kati ya zilizoorodheshwa walivyojitokeza kupambana na maadui hao.

**USHAIRI**

Diwani ya Mloka - C. Mloka (B.P.)
Diwani ya Ustadh - A. Andanenga (B.P.)
Malenga Wapya - Takiluki (DUP)

**RIWAYA**

Hiba ya Wivu - Z. Mwanga (R.P.)
Kusadikika - S. Robert (Nelson)
Zawadi ya Ushindi - B. Mtobwa (R.P.)

**THAMTHILIYA**

Hawala ya Fedha - A. Lihamba (T.P.H.)
Mfalme Juha - F. Topan (DUP)
Ngoswe - Penzi Kitovu cha Uzembe - E. Semzaba (ESC)

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org